# Mbunge wa Kilwa kusini awawekea dhamana wanamtandao.

- Ni Katika Kisa cha Mtendaji Kuwashitaki WANAMJUMITA.
- Mtendaji, mwekezaji waonja joto ya jiwe Mkutanoni

***Imetayarishwa na mwandishi wetu, Kilwa***

MBUNGE wa jimbo la Kilwa Kusini Mh. Selemani Saidi Bungara, amejitosa katika kesi inayowakabili wanachama wa MJUMITA kutoka mtandao wa MWATUKI, Kijiji cha Ruhatwe kata ya Kisangi wilayani Kilwa.



Kesi hiyo ya aina yake ilifunguliwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Ruhatwe dhidi ya wananchi nane na kuwafikisha polisi kwa madai ya kuvuruga mkutano mkuu wa kijiji uliolenga kuridhia maombi ya mwekezaji wa kampuni moja ya kichina ambayo ilitaka sehemu ya ardhi ya kijiji kwa ajili ya shughuli za kilimo cha mahindi, mtama na mihogo.

Mwekezaji huyo alifika kijijini hapo kuomba ardhi akiwa ameambatana na Afisa ardhi wa wilaya kufuatia mipango yake ya awali ya kutaka ardhi katika kijiji hicho ku kwama baada ya wananchi kupinga maombi yake. Katika hali ya kutatanisha na ya kushangaza sana, ilidaiwa kuwa baadhi ya viongozi wa kijiji walijipanga kutumia mkutano huo kuendelea kuwashawishi wananchi kukubali maombi ya awali ya muwekezaji huyo ambayo hata hivyo yalishakataliwa na wananchi katika mkutano mkuu wa kijiji. Katika mkutano huu wa dharura ambao uliitishwa tarehe 22/10/2011 saa 11 jioni ulizusha sintofahamu vichwani mwa baadhi ya wanachama wa MJUMITA na wananchi wengine waliokuwa mkutanoni hapo na kuwalazimu kuhoji uhalai wa kuuita mkutano huo wa dharura wakati unahusisha jambo linalowahusu wanakijiji wote, na kwamba kuna udharura gani kwenye uwekezaji wa kilimo!!!

Aidha nguvu ya WANAMJUMITA hao kuhoji uhalali wa mkutano huo wa dharura tena jioni ya saa 11, ilichangiwa na mjadala kuhusu uwekezaji usiofuata utaratibu ulioibuka katika Mkutano Mkuu wa mtandao wa MWATUKI uliofanyika kijijini Ruhatwe na kuhudhuriwa na viongozi wa MJUMITA kanda ya kusini. Katika mkutano huo, wananchi walitahadharishwa kuhusu madhara ya kutoa ardhi ya misitu yao kwa wawekezaji bila kufuata kanuni zilizowekwa kisheria.

Hata hivyo pamoja na viongozi kadhaa wa kijiji hicho kuwashawishi wananchi kukubali maombi ya muwekezaji huyo kwa kivuli cha "demokrasia" baadhi ya wananchi walioshiriki mkutano huo walipiga kelele kuwa mkutano huo ubatilishwe kwa kuwa haukukidhi vigezo vya kuitwa mkutano mkuu, kwani serikali ya kijiji haikupata muda wa kutosha kuwajulisha wananchi wote na kwamba uliitishwa jioni muda ambao haujazoeleka na hivyo wananchi wengi hawakuweza kufika, na hivyo hicho kilichoitwa demokrasia kingekuwa danganya toto.

Iliulazimu uongozi wa kijiji uahirishe mkutano huo hadi kesho yake tarehe 23/10/2011. Hata hivyo baadhi ya

wananchi walimpa wakati mgumu mwekezaji huyo na uongozi wa kijiji na waliendelea kukataa kwa nguvu zote maombi ya mwekezaji huyo. Baadhi yao walienda mbali zaidi na kuhoji uhalali wa serikali ya kijiji kuitisha mkutano huo wakati haikuwahi kuitisha mkutano mkuu wa kijiji kwa takribani miaka miwili iliyopita, hatua iliyopelekea kuvurugika kwa mkutano huo.

Kufuatia kuvurugika kwa mkutano huo, Afisa Mtendaji wa kijiji aliamua kuwafikisha polisi wanakijiji wapatao nane wakiwemo wanachama wa MJUMITA akiwahusisha kuwa chanzo cha vurugu katika kwenye mkutano wa kijiji na kupelekea mkutano halali kuvunjika.

Wananchi hao walimuomba Mbunge wao aingilie kati na kukubali kufika polisi ili awasaidie kuhusu taratibu za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwawekea dhamana. Mbunge huyo alimshawishi Afisa Mtendaji huyo pamoja na OCD kukubali kufuta kesi hiyo na kuirudisha kijijini na akaahidi kushiriki kusuluhisha.

Katika siku za hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la uwekezaji usiofuata taratibu katika wilaya ya Kilwa kama ilivyo katika sehemu nyingi za Tanzania, jambo linalohatarisha mustakabail ya uwezo wa jamii ya wazalendo kumiliki na kunufaika na raslimali zilizopo katika nchi yao, hususani ardhi.